# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

***Dodoma***
***20 Novemba, 2025***

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amezindua rasmi Tume Huru ya Uchunguzi ya Matukio ya Uvunjifu wa Amani yaliyotokea wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa tarehe 29 Oktoba, 2025.

Rais Dkt. Samia aliunda Tume hiyo tarehe 18 Novemba, 2025 kwa mujibu wa Sheria ya Tume za Uchunguzi ya mwaka 2023 (Sura ya 32). Tume itakuwa chini ya uenyekiti wa Jaji Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Mohamed Chande Othman, na imepewa muda wa miezi mitatu ya utekelezaji wa jukumu hilo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi, Rais Dkt. Samia amewashukuru wajumbe wa Tume kwa kukubali jukumu hilo muhimu kwa maslahi ya Taifa na kusisitiza kuwa ana imani na uwezo wao wa kulitekeleza jukumu hili kubwa kwa weledi na uadilifu.

Halikadhalika, alisema Tume itapatiwa hadidu za rejea ikiwemo uchunguzi wa kina wa chanzo cha matukio hayo, mienendo ya wadau mbalimbali wa siasa na jamii, pamoja na hatua zilizochukuliwa kukabiliana na vurugu hizo na mazingira yaliyohatarisha amani na kusababisha madhara kwa wananchi na Serikali.

Katika hatua nyingine, alisisitiza kuwa kazi na mapendekezo ya Tume hiyo yataweka msingi kuelekea uundwaji wa Tume ya Mazungumzo na Maridhiano kama alivyoahidi kuiunda katika siku 100 za mwanzo za muhula wa pili wa uongozi wake.

Rais Dkt. Samia amesema kwamba uamuzi wa kuunda Tume ya ndani umetokana na umuhimu wa Taifa kujitathmini lenyewe na kwamba mapendekezo yake yatatoa dira muhimu ya kusonga mbele kama Taifa linalothamini amani, utulivu na mshikamano.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu